

# **HOTUBA YA DG SIKU YA UHISITI WA KCGS INAYOFANYIKA KATIKA KAUNTI TANO ZA PWANI (KWALE,MOMBASA,KILIFI,TANA RIVER NA LAMU)MWAKA WA 2024.**

Mheshimiwa gavana/mwakilishi,

kamishna wa kaunti

wakurugenzi wa kaunti

wanachama wa BMU na itifaki zote zimezingatiwa,

*Salam Aleikum!*

Nachukua fursa hii kuwakaribisha sana kwa kikao hiki cha siku ya uhamasishaji wa **KCGS**. Ni heshima na fursa nzuri kusimama hapa leo na kuwasiliana nanyi nyote. Kama **DG**, ningependa kuanza kwa kutoa shukrani zangu kwa usaidizi na faraja ambayo **KCGS** imepokea kutoka kwa washikadau tofauti waliopo hapa. Imekuwa ya kufana sana na ninashukuru kila mmoja wenu kutoka ndani ya moyo wangu kwa kujitolea na kutenga muda na kujumuika nasi siku ya leo. Ulinzi na Usalama wa Baharini ni jukumu la **KCGS** na kwa hivyo tunajitahidi kila siku kuhakikisha kuwa eneo letu la bahari linakuwa zuri na endelevu kwa shughuli mbalimbali zikiwemo za uvuvi na usafirishaji. Tunahakikisha kuwa shughuli hizi zinafanyika kwa urahisi kupitia ushirikiano na wadau mbalimbali na muhimu zaidi jamii ya wavuvi. Uvuvi kama sekta katika **UCHUMI SAMAWATI** ina uwezo mkubwa katika uzalishaji wa uchumi wa nchi yetu, hata hivyo kutokana na baadhi ya changamoto, imekuwa vigumu kutimiza kikamilifu uwezo huu. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja na uharamia, uchafuzi wa

mazingira haswa bahari, na ukosefu wa mafunzo sahihi kwa wavuvi wetu kuhusu mbinu za kukaa baharini.

**KCGS** ingependa kuwashukuru washirika wetu **Go blue** kwa usaidizi wao mwafaka kwani wamekua muhimu katika kuimarisha utoaji wa huduma katika **KCGS** kama moja wapo ya hatua za kusaidia kujenga uwezo wetu pamoja na wadau katika sekta ya bahari. Hili limeleta ushirikiano bora wa jamii. Mpango huu wa **STF** umepunguza kwa kiasi kikubwa matukio ya wavuvi kupotea na hata kupoteza maisha yao baharini kwa kuwapa stadi muhimu za kuweza kijiokoa wakati wa tukio au dharura. Kando na uundaji wa programu hii ya Mafunzo ya Usalama kwa Wavuvi **STF**, washirika wetu wameweza pia kutengeneza **Usalama Baharini Coastal App**. Ninajivunia kusema kwamba programu hii ni ya kwanza duniani kote kutengenezwa na kwa hivyo inaiweka Kenya katika mstari wa mbele katika masuala ya usalama wa baharini. Kwa furaha kubwa nasimama mbele yenu kuwaarifu kuwa tunazindua rasmi programu hii. Itatumiwa na wavuvi na mwananchi kuripoti matukio yakiwemo; uvuvi haramu, shughuli haramu baharini, shughuli haramu kwenye ufuo, uchafuzi wa bahari na shughuli za utafutaji na uokoaji.

Nawahimiza nyote muwe sehemu ya shughuli hii muhimu ya kuongeza manufaa kwa jamii yetu kupitia mpango wa **STF** kwa wavuvi na kwa kutumia **USALAMA BAHARINI APP**.

***Asanteni sana.***